WIZARA YA NISHATI

# NewsBulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 69 | Agosti 1 - 31 2025



# AGIZO LA MINADA YOTE NCHINI KUTUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA LAANZA KUTEKELEZWA

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI


**MWENYEKITI**

Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**

Dkt. James Mataragio

**MHARIRI**

Neema Chalila Mbuja
Teresia Mhagama

**WAANDISHI**

Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Felista Charles

**WAPIGA PICHA**

Henry Kilasila
Godfrey Mwemezi
Ruben Richard
Amanzi Kimonjo

**MSANIFU KURASA**

Brian Mbaga



© NISHATI 2025

# AGIZO LA MINADA YOTE NCHINI KUTUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA LAANZA KUTEKELEZWA

- Wachoma nyama na Mama Lishe katika mnada wa Msalato Dodoma waanza kuonja matunda ya Nishati Safi ya Kupikia
- Dkt. Biteko asema ni matunda ya Rais, Dkt. Samia ambaye anafahamu machungu ya kutumia Nishati isiyo safi ya Kupikia
- Atoa maagizo kwa Mkurugenzi Jiji la Dodoma kuweka miundombinu itakayohakikisha majiko ya Nishati Safi ya Kupikia ya Wachoma nyama yanakuwa salama
- Apongeza REA, Wizara ya Nishati kutekeleza agizo alilolitoa: STAMICO yatakiwa kuweka kituo cha kudumu cha mkaa mbadala Mnada wa Msalato
- Kituo kikubwa cha kusambaza umeme na kusimamia gridi ya Taifa kujengwa Dodoma

Agizo la Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko kwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuhakikisha kuwa minada yote nchini inakuwa na miundombinu itakayowawezesha Wachoma nyama, Mama Lishe na Baba Lishe kutumia nishati Safi ya Kupikia limeanza kutekelezwa ikiwa ni utekelezaji wa ajenda ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha wananchi wote wanatumia Nishati iliyosafi ya kupikia.

Safari ya kuhakikisha minada yote nchini inatumia nishati safi ya kupikia, imeanzia katika Mnada wa Msalato jijini Dodoma, Dkt. Biteko amegawa majiko banifu kwa Mamalishe takriban 27 wanaohudumu katika mnada huo pamoja na majiko ya kuchomea nyama.

"Kama mnavyofahamu, Mhe. Rais alitoa maelekezo kuwa watanzania asilimia 80 ifikapo 2034 watumie nishati safi ya kupikia, maelekezo yake yanaendelea kutekelezwa, tulianza na taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 kuondoa matumizi ya kuni na mkaa ikiwemo magereza yote nchini, shule za Sekondari , vyuo na taasisi nyinginezo lakini moja ya maeneo



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akikabidhi jiko kwa Mama Lishe katika mnada wa Msalato Dodoma.

yaliyobaki ni pamoja na minada ambayo inahudumia watu wengi." Amesema Dkt.Biteko

Dkt. Biteko ameeleza kuwa kazi ya kufunga mifumo ya Nishati Safi ya Kupikia kwenye minada ilianza na utafiti ili kupata hali halisi ya matumizi ya nishati hiyo ambapo katika utafiti huo, asilimia 89.5 ya wachoma nyama wote walisema hawana uelewa kuhusu nishati safi ya kupikia, pia utafiti huo umeonesha asilimia 26.3 ya wachoma nyama wamewahi kutumia nishati safi ya kupikia na asilimia iliyobaki haijawahi kutumia. Hii ikionesha kuwa bado kuna kazi ya kufanya kuelekea kwenye matumizi ya Nishati Safi ya kupikia.

Amesisitiza kuwa, hatua hizo zinazochukuliwa na Serikali katika Nishati Safi ya Kupikia, ni matunda ya Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amejipambanua kama kiongozi mwanamke anayejua machungu ya matumizi ya nishati isiyo safi na wakati wote anaelekeza kuwa yeye anachotaka kuona ni watu wengi hawatumii nishati isiyo safi



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akitembelea baadhi ya wachoma nyama

ya kupikia.

Ameongeza kuwa, Tanzania ndiyo nchi nchi pekee barani Afrika ambayo imezindua Mkakati wa Taifa wa matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ambao umekuwa ni mfano barani Afrika na nchi nyingine zinakuja kujifunza hivyo lazima iwe mfano na kinara kwa kuishi yale inayoyasema.

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko amemuagiza Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma kuweka miundombinu ambayo itafanya majiko ya nishati safi ya kupikia katika minada mkoani Dodoma kuwa katika sehemu ya kudumu na zoezi hilo lianze mara moja.

Aidha, ameliagiza Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kuweka kituo cha kudumu cha kuuza mkaa mbadala katika mnada wa Msalato ili wananchi wasikwame pale wanapohitaji nishati hiyo.

Vilevile ameitaka REA, kuhakikisha majiko makubwa ya kuchomea nyama ambayo yanatumia Nishati Safi ya Kupikia yanapatikana ili wananchi wanaochoma nyama na wanaofuata huduma wasipoate madhara ya afya kuanzia sasa kwenda mbele.

Dkt. Biteko ameipongeza REA na Watendaji wa Wizara ya Nishati kwa kupoeka agizo lake kwa haraka na kulifanyia kazi, pia amewaasa kuendelea na ubunifu utakaowawezesha wananchi kutumia nishati safi ya kupikia na wasisahau kufanya tathmini ya matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia katika minada hiyo.

Pia, amewaasa Mama lishe na Baba lishe kuiunga mkono ajenda ya nishati safi ya kupikia na kuwa mabalozi wa nishati hiyo kwani watu wakiona faida zinazotokana na kutumia nishati safi ya kupikia kutoka kwao nao watavutika kuitumia.

Dkt. Biteko amemshukuru Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kufanya kazi kubwa ya mfano katika sekta ya Nishati ambapo amesema Mkoa wa Dodoma muda si mrefu utakuwa ni kitovu cha usambazaji umeme katika mikoa mbalimbali ikiwemo Singida, Shinyanga, Tabora, Kigoma na Arusha na pia kitajengwa kituo kikubwa cha kusambaza umeme na kusimamia gridi ya Taifa.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule amesema walaji katika mnada wa Msalato kwa wiki ni kati ya 2000 na 3000 hivyo kwa kutumia Nishati Safi ya Kupikia itawezesha kuokoa mazingira kwa kuondokana na kuni na mkaa ambao ulikuwa ukitumika kuhudumia idadi hiyo ya watu.

Aidha ameomba a kampeni hiyo ya Nishati Safi ya Kupikia ifike kwenye masoko mbalimbali ambayo ina mama lishe na baba lishe.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amemshukuru Dkt. Biteko kwa maono yake ambayo yamewezesha Mnada wa Msalato kufikiwa na Nishati Safi ya Kupikia ikiwa ni mwanzo wa kusogeza huduma kwenye minada mingine.

Ameeleza kuwa kiwango cha matumizi ya nishati safi ya kupikia kimepanda kutoka asilimia 6.9 ya mwaka 2022 na hadi kufikia asilimia 20.3 na kusema kuwa kwa jinsi matumizi ya nishatil safi ya kupikia yanavyoongezeka Serikali itatimiza lengo lake ya kufikisha Nishati Safi ya Kupikia kwa watanzania wapatao asilimia 80 kama alivyoagiza Mhe.Rais.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Hassan Saidy amesema mnada wa Msalato una wachoma nyama kati ya 45 na 50 ambao watapatiwa majiko makubwa ya kuchomea nyama, pia kuna mama lishe 27 ambao tayari wote wamepatiwa majiko banifu.

Mwenyekiti wa Wachoma nyama katika Mnada wa Msalato, Mathias Raphael amesema baada ya kupata elimu ya nishati safi ya kupikia katika mnada huo ameanza kutumia jiko linalotumia mkaa mbadala ambao amesema kuwa unatumika kidogo huku ukichoma nyama nyingi, unakaa muda mrefu na hauna moshi.

# DKT. BITEKO AZINDUA PROGRAMU YA UGAWAJI MAJIKO YA UMEME KWA BEI YA RUZUKU KWA WAFANYAKAZI WA TANESCO

- Lengo ni kuchochea Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia
- Asema matumizi ya umeme kwa ajili ya kupikia ni nafuu zaidi ukilinganisha na mkaa; Wananchi wahamasike
- Awapongeza TANESCO kutekeleza maoni ya Rais Samia kwa vitendo



Imeelezwa kuwa, matumizi ya nishati safi ya kupikia ni ajenda ya kitaifa inayolenga kuhamasisha wananchi kutumia nishati safi na salama ya kupikia ikiwemo nishati ya umeme.

Aidha, takwimu za mwaka 2022 zinaonesha kuwa Watanzania wanaotumia nishati ya umeme kwa ajili ya kupikia ni asilimia 4.2 tu huku ikitajwa kuwa idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya watanzania waliopo.

Akizungumza jijini Dodoma wakati akizindua Mpango wa Ugawaji Majiko ya Kupikia kwa Umeme kwa Wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa kutokana na historia ya siku za nyuma Watanzania walidhani kuwa kupika kwa umeme ni ghali zaidi tatizo ambalo lilisababishwa na masuala mengi ikiwemo elimu kuhusu unafuu wa gharama kwa matumizi ya umeme.

“Utafiti wa TANESCO unaonesha kuwa kupikia kwa nishati ya umeme, hasa kwa kutumia majiko janja yenye ufanisi ni nafuu zaidi kuliko wanavyofikiria wengi miongoni mwetu katika jamii tunazoishi. Utafiti huo unaonesha kuwa, majiko janja ya umeme yanaweza kutumia chini ya uniti moja (1) ya umeme ambayo ni sawa na chini ya shilingi za Kitanzania 352 kuandaa mlo mmoja,” amesema Dkt. Biteko.

Amefafanua kuwa matumizi ya umeme kwa ajili ya kupikia ni nafuu kuliko nishati nyingine hivyo Watanzania hawana haja



ya kuogopa kutumia umeme. Aidha, hatua ya Ugawaji Majiko ya Kupikia kwa Umeme kwa Wafanyakazi TANESCO itakuwa hatua muhimu katika mabadiliko kwa kuwa wafanyakazi hao wa TANESCO watakuwa mabalozi wa matumizi ya nishati safi ya kupikia hususan majiko ya umeme katika jamii.







# DKT. BITEKO ATAKA WATUMISHI WIZARA YA NISHATI NA TAASISI ZAKE KUWA MFANO WA MATUMIZI NISHATI SAFI YA KUPIKIA

- Lengo ni kutekeleza Ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia kwa vitendo
- Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia yapaa kutoka asilimia 6 hadi 20.3



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akimkabidhi jiko mtumishi mmoja wa Wizara ya Nishati.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, amewataka watumishi katika Wizara ya Nishati na Taasisi zilizochini ya wizara hiyo kuwa mfano katika matumizi ya Nishati Safi ya kupikia ili kuitekeleza kwa vitendo ajenda iliyoasisiswa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan inayolenga kuhamasisha matumizi ya nishati safi na salama kwa afya

Maelekezo hayo ameyatoa jijini Dodoma wakati akigawa majiko yanayotumia umeme kidogo kwa watumishi wa Wizara ya Nishati na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ambapo amewataka Watumishi hao wawe mabalozi katika kutekeleza ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia.

“ Leo tunagawa majiko haya kwa kuwa nyinyi ndiyo wenye dhamana kuu ya kutekeleza Ajenda ya Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia hivyo wajibu wenu ni mabalozi wazuri kwa watu wanaowazunguka ili nao



Watumishi mbalimbali wa wizara ya Nishati katika hafla ya ugawaji wa majiko.

wahamasike kutumia nishati hii safi." Amesema Dkt. Biteko

Amesema kufuatia mwamko mkubwa unaoendelea sasa kwa wananchi kufahamu faida za matumizi ya nishati safi ya kupikia, kiwango cha watumiaji kimepanda kutoka asilimia 6 na kufikia asilimia 20.3 huku lengo likiwa ni kufikia asilimia 80 ifikapo 2034.

Dkt. Biteko ametanabaisha kuwa Idadi ya watu wanaoendelea kutumia nishati isiyo safi na salama ya kupikia bado ni kubwa duniani, barani Afrika na hapa Tanzania hivyo ni jukumu la watumishi wote wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake kuhakikisha watanzania wanapata elimu sahihi ili waweze kubadilika na kufikia lengo lililokusudiwa.

Akigawa majiko 220 kwa watumishi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Dkt. Biteko amepongeza Taasisi hiyo kwa kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia hususan katika maeneo ya vijijini ambapo kumeonekana kuwa bado changamoto ya kufikiwa na Nishati Safi ya Kupikia.

Pia ameipongeza REA kwa kuhakikisha Vijiji vyote 12,318 nchini vinafikiwa na umeme.

Kwa Upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mhandisi Felchesmi Mramba amemhakikisha Dkt. Biteko kuwa atakahikisha agizo alilolitoa linatekezwa na Taasisi zote anazozisimamia.

Amesema atahakikisha kwamba Ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia yanafikia malengo yaliyokusudiwa.

Amewasisitiza watumishi kutumia Majiko hayo waliyopewa na si kuyahifadhi.

# DKT. BITEKO AHIMIZA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO VIKAO VYA KIMKAKATI VYA WENYEVITI WA BODI NA WAKUU WA TAASISI

- Awakumbusha kuhusu dhamana waliyobeba ya kubadili maisha ya watanzania kupitia mtaji wa shilingi Trilioni 86 waliopewa
- Afunga Kikao kazi cha Tatu cha Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi
- Asema Rais, Dkt. Samia anatambua mchango wa Taasisi za umma; ana matarajio makubwa kutoka kwao
- Awakumbusha kutekeleza Maagizo yaliyotolewa na Makamu wa Rais
- Kikao kazi chafanyika kwa mafanikio; chahusisha washiriki zaidi ya 600



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akiwahimiza Wenyeviti na Wakuu wa Taasisi za Umma nchini kusimamia utekelezaji wa maazimio ya kimkakati yanayofikiwa katika vikao kazi wanavyofanya kwa kutambua kuwa wamebeba dhamana ya kuboresha maisha ya Watanzania kupitia mtaji wa shilingi Trilioni 86 ambao Serikali imewekeza kwenye Taasisi na mashirika yake.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewahimiza Wenyeviti na Wakuu wa Taasisi za Umma nchini kusimamia utekelezaji wa maazimio ya kimkakati yanayofikiwa katika vikao kazi wanavyofanya kwa kutambua kuwa wamebeba dhamana ya kuboresha maisha ya Watanzania kupitia mtaji wa shilingi Trilioni 86 ambao Serikali imewekeza kwenye Taasisi na mashirika yake.

Dkt. Biteko ameyasema hayo jijini Arusha wakati akifunga kikao kazi cha Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma (CEOs FORUM 2025).

"Watanzania wanawategemea ninyi kuwabadilishia maisha, kama tunazungumza kuhusu umaskini wa watu, Serikali inapaswa kuwa kiongozi wa kuwaondolea watu umaskini wao, hivyo hamna budi kutambua kuwa mnalo deni la kuboresha hali zetu na maisha yetu." Amesema Dkt. Biteko.

Dkt. Biteko amewahakikishia Watendaji hao kuwa Serikali katika ngazi zote inatambua mchango wa taasisi na mashirika katika ukuaji wa uchumi na pia inatambua mchango wa vikao kazi vya watendaji hao ambavyo vimepelekea mashirika kuongeza mchango wake katika mfuko mkuu wa Taifa.

" Vikao kazi hivi mnavyofanya vimeonesha mchango wake katika uchumi, mfano katika kikao kazi cha mwaka 2024 mliazimia mashirika ya umma yaboreshe utendaji na kuongeza uchangiaji katika mfuko mkuu wa Serikali na matokeo yameonekana mfano Shirika la Maendeleo ya Petroli ( TPDC) liliongeza uchangiaji wake kwa asilimia 100, shirika hili liliongeza uchangiaji wake kutoka shilingi bilioni 5.5 kwa mwaka 2023/2024 hadi shilingi bilioni



Picha ya Pamoja ya Kikao kazi cha Tatu cha Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi kilichofanyika Jijini Arusha.

11.1 mwaka 2024/2025." Amesema Dkt.Biteko

Ameongeza kuwa, uchagiaji wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) umeongezeka kwa asilimia 363 katika mfuko mkuu wa Serikali ambapo NHC ilichangia shilingi bilioni 1.2 mwaka 2023/ 24 na mwaka 2024/2025 ilichangia shilingi bilioni 5.5.

Dkt. Biteko amewaeleza Wenyeviti wa Bodi na Wakuu wa Taasisi kuwa "Rais Samia pamoja na kuthamini mchango wenu kwa Serikali anatarajia mengi kutoka kwenu na Watanzania wana matarajio makubwa hasa wakati tukielekea kwenye utekelezaji wa Dira 2050, endeleeni kuongeza mchango wenu kwenye ukuaji wa uchumi, mjitegemee na muwe mfano wa taasisi binafsi."

Katika.hatua nyingine, Dkt. Biteko ametaka viongozi hao kufanyia kazi agizo lililotolewa na Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango la kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato.

Pia amempongeza Msajili wa Hazina kwa kuwa na maono ya kuratibu kikao kazi hicho ili kujadili masuala yatakayosukuma mbele utendaji wa taasisi.

Katika hafla hiyo, Dkt. Biteko hakuacha kukumbusha kuhusu ushiriki wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ambapo amesema uchaguzi huo uwe ni ajenda ya watu wote wakiwemo Wenyeviti wa Bodi na Wakuu wa Taasisi hivyo waone kuwa wana wajibu wa kuwasisitiza watu kwenye taasisi zao kujitokeza kusikiliza wagombea na baadaye kupiga kura kwa amani kwani kukiwa na amani mashirika hayo pia yatafanya vizuri zaidi.

Naibu Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Mhe. Stanslaus Nyongo kwa upande wake, amemshukuru Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dira na muongozo katika kuendeleza mashirika ya umma ili yaweze kuwa na tija nchini.

Amesema katika siku tatu za kikao kazi washiriki wamejifunza na kubadilishana uzoefu kupitia watoa mada wa ndani na nje ya nchi waliobobea.

Amesema Wizara ya Mipango na Uwekezaji itahakikisha maazimio ya kikao kazi hicho yanatekelezwa ipasavyo, pia Wizara itasimamia mageuzi ya kuhakikisha mashirika ya umma yanachangia ukuaji wa pato la taifa hadi kufikia Dola za Marekani trilioni 1 ifikapo 2050 ambapo kwa sasa pato la taifa ni dola za Marekani bilioni 85.

Kwa upande wake Salim Kali, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Arusha amesema wilaya 6 za Mkoa wa Arusha zimefikiwa na umeme hadi ngazi ya vijiji, pia miradi ya maji imefanyika pamoja na miundombinu ya Barabara ambayo imewezesha maisha bora kwa watu wa aina zote wakiwemo watalii.

Awali, Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu alisema kuwa katika kikao kazi hicho kampuni zaidi 300 zimeshiriki huku washiriki wakiwa ni zaidi ya 650.

Alisema kikao kilikuwa na majadiliano mbalimbali ya kina yanayolenga kusukuma mbele uchumi wa nchi na kusimamia uwekezaji wa Serikali kwa taasisi za umma wa zaidi ya shilingi trilioni 86.

Mkutano huo wa Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma uliongozwa na kaulimbiu ya "Ushirikiano Endelevu wa Kibiashara katika Mazingira Shindani Kimataifa-Nafasi ya Mashirika ya Umma."

# AHADI YA SERIKALI KUFIKISHA UMEME WA GRIDI KAGERA YATEKELEZWA

- Dkt.Biteko ashuhudia utiaji saini mikataba itakayowezesha Wilaya zote Kagera kupata umeme wa Gridi
- Awali umeme mwingi ulikuwa ukitoka nchini Uganda hivyo kufanya Mkoa kutokuwa na umeme wa uhakika na wa kutosha
- Asema Rais.Dkt. Samia alishatoa maagizo ya mradi huo kutekelezwa kwa wakati na kwa usahihi
- Aagiza wananchi 1,014 waliopisha mradi kulipwa fidia kuanzia mwezi Septemba 2025
- Apongeza Wizara ya Nishati na TANESCO kwa ufanisi katika usimamizi wa miradi



Dkt. Biteko akiwashukuru wafadhili wa mradi ambao wametoa Dola za Kimarekani takriban milioni 105.6 ambazo ameagiza kuwa zitumike kwa usahihi ili kuwapa sababu wafadhili wengine kuendelea kusaidia miradi mbalimbali.

Ahadi ya Serikali ya kufikisha umeme wa gridi ya taifa katika Wilaya zote za Mkoa wa Kagera imetekelezwa baada ya Serikali kusaini mikataba ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Benako, Ngara hadi Kyaka wilayani Misenyi na kituo cha kupoza umeme cha Benako cha msongo wa kilovoti 220/33, hatua inayotoa uhakika kwa Mkoa huo sasa kupata umeme wa gridi

badala ya kutegemea umeme kutoka Uganda kwa kiasi kikubwa.

Akizungumza baada ya kushuhudia utiaji saini kwa mikataba hiyo jijini Dodoma Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa kuanza kutekelezwa kwa mradi huo ni moja ya maelekezo ya Dkt.Samia Suluhu Hassan ambaye alikuwa na kiu ya kutekeleza ahadi ya Serikali kwa wananchi wa Kagera ya kupata umeme wa uhakika muda wote ili kutekeleza shughuli zao za kiuchumi na kijamii.

" Kupitia mradi huu, Mkoa wa Kagera kwa mara ya kwanza na wenyewe unaingia kwenye gridi ya Taifa hasa na hivyo kuongeza uhakika wa upatikanaji wa umeme hususan katika Wilaya za Bukoba, Muleba, Misenyi, Karagwe, Kyerwa na maeneo mengine ya jirani, nawahakikishia watu wa Kagera kuwa Serikali imeshaamua mradi huu ufanyike kwa wakati kwa miezi 24 tu" Amesema Dkt. Biteko.

Dkt. Biteko amesema, Kagera ambayo mahitaji yake ya umeme hayazidi megawati 47 baada ya muda itakuwa na uhakika mkubwa wa upatikanaji umeme kwani kutakuwa na njia mbalimbali za kufikisha umeme mkoani humo ikiwemo Benako- Karagwe hadi Kayaka, Nyakanazi- Biharamulo hadi Muleba na kuna mradi mwingine mkubwa unaotarajiwa kujengwa kutoka Ibadakuli hadi Mbarara Uganda wa kV 400. Vilevile kuna mradi wa uzalishaji umeme wa Kakono wa megawati 87 ambao upo katika hatua za mwisho za kutafuta Mkandarasi.

Ameongeza kuwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan pia anaendelea kutekeleza miradi mingine ya umeme katika maeneo mengine ikiwemo mradi wa usafirishaji umeme wa kV 400 wa Tanzania-Zambia, mradi wa Usafirishaji umeme wa kV 400 Chalinze-Dodoma , mradi wa usafirishaji umeme wa Mkuranga -Pwani ambao utapeleka umeme kwa wananchi wa Kusini, pia mradi wa usafirishaji umeme wa gridi imara wa Tunduru- Masasi- Mahumbika ambao pia unaenda kutoa uhakika wa umeme katika mikoa ya Kusini.

" Utekelezaji wa miradi hii yote ya umeme ni kielelezo kuwa, Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshaonesha njia ya kuwafikishia wananchi umeme wa uhakika sasa kinachohitajika kwa watendaji ni kukimbia badala ya kutembea kwani kinachotakiwa ni matokeo na siyo kusema sana." Amesisitiza Dkt. Biteko

Pia Dkt. Biteko amewashukuru wafadhili wa mradi ambao wametoa Dola za Kimarekani takriban milioni 105.6 ambazo ameagiza kuwa zitumike kwa usahihi ili kuwapa sababu wafadhili wengine kuendelea kusaidia miradi mbalimbali.

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko ameagiza TANESCO kuhakikisha wananchi 1,014 wanaopisha mradi wanalipwa fidia yao mapema iwezekanavyo yaani kuanzia mwezi septemba mwaka huu.

Aidha, amempongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga na watendaji wa TANESCO kwa kuendelea kusimamia kwa umakini Sekta ya Nishati.

Vilevile, ameipongeza TANESCO kwa kuendelea kuboresha utendaji wake na kwa kusimamia haki hasa pale zabuni zinapotangazwa. Aidha ametaka mipango iliyowekwa kwenye mradi huo iheshimiwe ili thamani ya fedha ionekane na wananchi wapate huduma kwa wakati.

Dkt. Biteko ameomba wananchi mkoani Kagera kuchangamkia fursa kutokana na kuwepo kwa umeme wa uhakika mara baada ya miradi itakayofikisha umeme mkoani humo kukamilika.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatuma Mwassa amepongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutekekeza mradi huo wenye gharama kubwa ikiwa ni kuonesha kwa vitendo jinsi inavyowajali wananchi hao.

Amesema wilaya zote mkoani Kagera zitaunganishwa na gridi kwani kwa sasa no wilaya tatu tu ndio zimeunganishwa na Gridi ya Taifa.

Ameahidi kuwa, Wananchi katika mkoa huo watakuwa watumiaji wazuri wa umeme na walipaji bili wazuri iili TANESCO iendelee kupata mapato ya kutekeleza miradi mingine l.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amesema Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa mikoa minne ambayo haijaunganishwa kwenye gridi ya Taifa ikiwemo Rukwa, Lindi na Mtwara.

Amesema tukio la leo ni la kihistoria kwani kukamilika kusainiwa kwa mikataba hiyo kunafanya mikoa yote iliyo nje ya gridi kuwa kwenye mpango wa kupelekewa umeme gridi hivyo kwa sasa hakuna mkoa ulio nje ya gridi ambao hauna mradi wa kupelekewa umeme.

Amesema kwa sasa Mkoa wa Kagera unapata umeme wa megawati 40 kutoka nchini




Picha ya Pamoja ya viongozi mbalimbali katika hafla kusaini mikataba ya ujenzi wan jia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Benako, Ngara hadi Kyaka wilayani Misenyi na kituo cha kupoza umeme cha Benako cha msongo.

Uganda kupitia kituo cha Kyaka na megawati 7 kutoka mwekezaji binafsi wa mradi wa Mirongo/ Kikagati.

Amesema wakati Serikali ya Awamu ya Sita inaingia madarakani jumla ya mikoa sita kati ya 26 haikuwa imeunganishwa kwenye gridi ya Taifa ila kwa kipindi cha minne Serikali imefanikiwa kuunganisha umeme Kigoma na Katavi huku mingine iiliyosalia ikiwa miaradi inayoendelea kutekekelezwa.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania ( TANZANIA), Lazaro Twange mradi huo una umuhimu mkubwa mkoani Kagera kwani wilaya za Kyerwa, Karagwe, Misenyi, Muleba, Bukoba Vijijini na Manispaa ya Bukoba kwa muda mrefu sasa zimekuwa zikiitumia umeme kutoka nchini Uganda takribani megawati 40 kupitia kituo cha kupoza umeme cha Kyaka ambacho kinapokea umeme kutoka Masaka, Uganda kupitia njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 132 kufuatia mkataba wa makubaliano baina ya Tanzania na Uganda.

Pia, kukamilika kwa mradi huo kutawezesha kuunganishwa kwa kituo cha kuzalisha umeme cha Kakono katika Gridi ya Taifa.

Amesema gharama za mradi ni shilingi bilioni 262.5 na utatekelezwa kwa muda wa miezi 24.

Amesema.Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ambapo Mfuko wa Maendeleo wa Shirika la Wauzaji Mafuta Duniani (OPEC) utachangia dola za Marekani milioni 60, Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi utachangia dola za Marekani milioni 30, Mfuko wa Maendeleo wa Saudia utachangia dola za Marekani milioni 13 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itachangia dola za Marekani milioni 2.6 kwa ajili ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi.

Amesema Wakandarasi watakaotekeleza mradi huo ni kampuni ya M/s. TBEA Co. Ltd kutoka nchini China ambayo itahusika na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Benako, na Kampuni ya M/s. Transrail Lighting Limited kutoka India itahusika na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Benako hadi Kyaka.

# WIZARA YA NISHATI YAJIVUNIA UTEKELEZAJI WA MIRADI SABA KATI YA 17 NCHINI

- Katibu Mkuu Nishati asema kati ya miradi hiyo saba, JNHPP imekamilika
- Asema EACOP imefikia asilimia 65 huku Serikali ya Tanzania ikichangia hisa za shilingi trilioni 1.12
- Ruhudji na Rumakali tafiti zakamilika



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba akielezea miradi ya kimkakati inayotekelezwa nchini Wizara ya Nishati ya Nishati nchini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba amesema kuwa katika miradi ya kimkakati inayotekelezwa nchini Wizara ya Nishati inatekeleza takribani miradi saba.

Mhandisi Mramba ameyasema hayo wakati wa uzinduzi wa Mpango wa Uwezeshaji wa Kiuchumi kwa Vijana (YEE) ambao unagusa maeneo yanayopitiwa na mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

"Miradi hiyo ni mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP), Mradi wa kugeuza gesi kuwa kimiminika (LNG), Mradi wa utafutaji mafuta, Miradi ya umeme ya Rumakali na Ruhudji na utafiti wa mafuta eneo la Mnazi Bay North", amesema Mha. Mramba.

Ameeleza kuwa katika miradi hiyo saba, mradi wa bwawa la kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere unaozalisha megawati 2,115 umekamilika na unaingiza umeme kwenye gridi ya Taifa.

Ameongeza kuwa mradi wa bomba la mafuta ghafi (EACOP) umefikia asilimia 65 na upo mbioni kukamilika, mradi wa LNG upo katika hatua za mwisho na miradi ya umeme ya Ruhudji na Rumakali tafiti zimekamilika.

Aidha, amesema Serikali ya Tanzania imeshachangia takribani shilingi trilioni 1.12 kwenye mradi wa EACOP kama hisa ya Tanzania katika mradi huo na kuna kampuni za kitanzania 200 ambazo zinatekeleza kazi mbalimbali katika mradi wa EACOP ambazo zitalipwa i jumla ya shilingi trilioni 1.325.

Mhandisi Mramba ametanabaisha kuwa mbali ya fursa za kiuchumi zinazopatikana pia wananchi wa maeneo ambayo mradi ya umeme inayopeleka umeme EACOP itapita watanufaika kwa kuunganishwa na huduma ya umeme.

# DKT.BITEKO AZINDUA TEKNOLOJIA YA KUONDOA UVIMBE MWILINI BILA UPASUAJI

- Ni kwa mara ya kwanza kufanyika Afrika Mashariki na Kati
- Aipa kongole Hospitali ya Kairuki kwa kutoa punguzo la asilimia 50 kwa wagonjwa 50 wa kwanza
- Asema Serikali itaendelea kuweka msukumo ushirikiano na Sekta binafsi
- Awaasa Watendaji Wizara ya Afya kutoogopa kujifunza pale Sekta binafsi inapofanya vizuri
- Wagonjwa 300 wanufaika na teknolojia ya utoaji uvimbe bila upasuaji



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizindua teknolojia ya kuondoa uvimbe mwilini bila upasuaji inayofahamika kama High-Intensity Focused Ultrasound (HIFU) katika Hospitali ya Kairuki ikiwa ni mara ya kwanza kwa huduma hiyo kuzinduliwa katika nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ameziindua teknolojia ya kuondoa uvimbe mwilini bila upasuaji inayofahamika kama High-Intensity Focused Ultrasound (HIFU) katika Hospitali ya Kairuki ikiwa ni mara ya kwanza kwa huduma hiyo kuzinduliwa katika nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Akizindua huduma hiyo jijini Dar es Salaam, Dkt. Biteko amepongeza Watendaji wa hospitali ya Kairuki pamoja na muasisi wake Hubert Kairuki na Mkewe kwa uthubutu wao katika masuala mbalimbali ikiwemo utoaji wa huduma hiyo ya HIFU ambayo imeiweka Tanzania katika rekodi ya kutoa uvimbe bila kufanya upasuaji barani Afrika suala ambalo pia litaongezea nchi mapato.

Ameeleza kuwa awali huduma ya HIFU barani Afrika likuwa ikipatikana katika nchi tatu tu ambazo ni Misri, Nigeria na Afrika Kusini.

Aidha, ameipongeza Hospitali ya Kairuki kwa kutoa punguzo la asilimia 50 la gharama za matibabu ya utoaji uvimbe bila upasuaji kwa

wagonjwa 50 wa kwanza ndani ya kipindi cha mwezi mmoja kuanzia leo ikiwa ni kielelezo cha Watendaji wa hospitali hiyo kuonesha utu kwa Watanzania, kuacha alama njema na kuunga mkono dhamira ya Serikali ya kutoa huduma kwa watanzania kwa gharama nafuu.

Dkt. Biteko amesema kuwa kufanyika kwa tukio hilo muhimu ni kielelezo cha Serikali ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuipa msukumo sekta binafsi na kuikuza ili kutoa huduma za matibabu kwa wananchi kwa ufanisi na kusogeza karibu huduma ambazo hapo awali zilikuwa hazipatikani ndani ya nchi hivyo ameahidi kuwa Serikali itaendelea kuunga mkono Sekta binafsi.

Aidha, ameipongeza Hospitali ya Kairuki kwa kuanzisha Idara ya huduma za dharura ambayo ina uwezo wa kuhudumia wagonjwa zaidi ya 9,000 kwa mwaka.

Katika hatua, nyingine, Dkt. Biteko amewataka Watendaji katika Wizara ya Afya kutoogopa kujifunza kutoka Sekta binafsi pale inapofanya vizuri na wawape ushirikiano wakati wote siyo nyakati za ukaguzi tu kwani lengo la Serikali ni kufikisha huduma bora kwa wananchi kwa ushirikiano wa Serikali na sekta hiyo.

Kuhusu ombi la Hospitali ya Kairuki la kujengewa barabara ya lami ya mita 300 kuelekea kwenye hospitali hiyo ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi ameelekeza Manispaa ya Kinondoni kufanyia kazi ombi hilo..

·

Dkt. Mwinyikondo Amir, kutoka Wizara ya Afya akimwakilisha Waziri wa Afya, amesema kuwa tukio hilo ni ishara ya ushirikiano uliopo kati ya sekta binafsi na Serikali katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Amesema Wizara ya Afya imekuwa na ushirikiano mkubwa na Hospitali ya Kairuki katika masuala mengi ikiwemo matumizi ya Bima ya Afya na kwamba pande zote mbili zinatambua kuwa zina wajibu wa kutekeleza dira ya maendeleo ya 2050 inayoelekeza uwepo wa jamii yenye afya bora.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Afya na Elimu Kairuki, Kokushubila Kairuki ameishukuru Serikali kwa kutambua mchango wa sekta binafsi katika kuboresha huduma za afya nchini.

Amesema sekta ya afya imekuwa na maendeleo makubwa chini ya uongozi wa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na kwamba hospitali hiyo itaendelea kuunga mkono juhudi hizo hasa ikiwa ni utekelezaji wa Dira 2050 inayolenga kujenga Taifa lenye uchumi imara na afya bora.

Amesema gharama za kuweka teknolojia hiyo ya HIFU ni shilingi Bilioni 12 na milioni 300.

Aidha amesema kutoka huduma ya HIFU ianze kutolewa tayari wananchi 300 wamepata huduma za uchunguzi huku 298 wakipata matibabu.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Kairuki, Dk. Onesmo Kaganda alisema uzinduzi wa HIFU ni tukio la kihistoria kwakuwa ni mara ya kwanza kwa huduma hiyo kuzinduliwa katika nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Amesema teknolojia hiyo barani Afrika imeanzishwa katika nchi tatu tu ambazo ni Misri, Nigeria na Afrika Kusini.

Ameeleza kuwa HIFU ni Teknolojia ya kisasa inayotumia Mawimbi Sauti (Sound Waves) b




Wageni mbalimbali waliohudhuria katika uzinduzi wa teknolojia ya kuondoa uvimbe mwilini bila upasuaji inayofahamika kama High-Intensity Focused Ultrasound (HIFU) jijini Dar es Salaam.

kutibu aina mbalimbali za uvimbe mwilini bila upasuaji, ikiwemo uvimbe wa saratani na usiokuwa wa saratani katika maeneo kama Matiti, Kongosho, Kizazi kwa Wanawake, na Tezi Dume kwa wanaume.

Ameeleza faida za huduma hiyo kuwa ni pamoja na kutokuwa na kovu kwa kuwa hakuna upasuaji, mgonjwa hawekewi nusu kaputi na mgonjwa hupona kwa muda mfupi na kurejea katika shughuli zake, matibabu hayahitaji kumwongezea damu mgonjwa hata kwa wagonjwa wenye upungufu wa damu, pia kupunguza gharama za kwenda nje ya nchi kutafuta matibabu.

Ameongeza kuwa, faida nyingine ya HIFU ni pamoja na tiba shufaa ambayo husaidia dawa za saratani kufanyakazi vizuri mwilini, kufubaza kukua kwa saratani mwilini (slowdown disease progression) na kupunguza maumivu kwa wagonjwa wa saratani.

Amesema mtambo huo ulianza kufanya kazi desemba 2023 ambapo mpaka sasa wagonjwa 303 wamefanyiwa uchunguzi na 298 kupatiwa matibabu na kumekuwa na matokeo chanya ya wagonjwa hao.

Amesema kuwepo kwa teknolojia hiyo ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya za kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii Tiba Kusini mwa jangwa la Sahara.

Pia, amemshukuru Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuweka mazingira wezeshi ya ushirikiano kati ya Serikali na Taasisi Binafsi.

Kuhusu Idara ya Huduma za Dharura iliyozinduliwa katika Hospitali ya Kairuki amesema itakuwa na uwezo wa kuhudumia wagonjwa zaidi ya 9000 kwa mwaka na pia imejizatiti kwa magonjwa ya dharura pindi yatakapotokea.

# WATANZANIA TUSIKUBALI UCHAGUZI UTUGAWE - DKT. BITEKO

- Asema Kuna Maisha baada ya Uchaguzi
- Amwakilisha Rais Samia,miaka 40 Kanisa Anglikana Dayosisi ya Kagera
- Rais Samia achangia Tsh. Milioni 50 Ujenzi wa Kanisa Dayosisi ya Kagera
- Anglikana Waishukuru Serikali, washirika wa maendeleo



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza na wananchi mbalimbali waliohudhuria katika Kilele cha Maadhimisho ya Miaka 40 ya Kuzaliwa kwa Dayosisi ya Kagera.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewataka Watanzania kuwapima wagombea wa nafasi mbalimbali katika Uchaguzi Mkuu ujao na kuchagua kwa haki ifikapo tarehe 29 Oktoba 2025 (mwaka huu) na katu wasikubali Uchaguzi uwagawe.

Dkt. Biteko amesema hayo wakati akimwakilisha Mheshimiwa Rais katika Kilele cha Maadhimisho ya Miaka 40 ya Kuzaliwa kwa Dayosisi ya Kagera iliyofanyika katika Viwanja vya Kanisa Kuu Yohana Mbatizaji - Murgwanza, Ngara.

Amesema kuwa watanzania wanayo haki ya kuwapima



Dkt. Biteko akimwakilisha Mheshimiwa Rais katika Kilele cha Maadhimisho ya Miaka 40 ya Kuzaliwa kwa Dayosisi ya Kagera iliyofanyika katika Viwanja vya Kanisa Kuu Yohana Mbatizaji - Murgwanza, Ngara.

wagombea kwa matendo yao na hatimaye kutenda haki kwa kufanya uchaguzi wao kwa njia ya demokrasia huku akisisitiza umuhimu wa kuzingatia kampeni za kistaarabu na kujiepusha na vitendo vya uvunjifu wa maadili.

Akiwasilisha salamu za Mheshimiwa Rais, Dkt. Biteko amesema Dkt. Samia anatambua na kuheshimu mchango wa taasisi za dini na mchango wake katika maendeleo ya Taifa. " Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mdau wa kujenga na kila mnachokifanya kinalenga katika maendeleo ya watu hivyo anaunga mkono jitihada za maendeleo ya wananchi," amesema Dkt. Biteko.

Katika kufanikisha azma yake, Rais Dkt. Samia amechangia shilingi milioni hamsini (50,000,000/=) katika harambee ya ujenzi wa Kanisa jipya la Anglikana Dayosisi ya Kagera.

Dkt. Biteko Amesisitiza umuhimu wa kila mtu kuwa kisababishi cha furaha kwa mwenzake ili kuwa na maisha ya ya furaha.

Awali, Askofu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Dayosisi ya Kagera, Darlington Misango Bendankeha ameishukuru Serikali kwa ushirikiano mkubwa unaopatikana katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Askofu Bendankeha amesisitiza kuwa Serikali katika ngazi zote inatoa ushirikiano na hivyo kufanikisha utekelezaji wa miradi ya Afya, Elimu kwa maendeleo ya jamii.

Ameiomba Serikali kufanikisha ujenzi wa Barabara inayounganisha taasisi mbalimbali za utoaji wa huduma yenye urefu wa mita 900, Gari la wagonjwa pamoja na mchango wa ujenzi Kanisa ambalo ujenzi wake unaendelea kwa gharama ya shilingi Bilioni 1.18

Kufuatia maombi hayo, Dkt. Biteko amemwelekeza Mkuu wa Mkoa, Mkuu Wilaya na Wakala wa Barabara mijini na vijijini (TARURA) kufanikisha ujenzi wa Kipande hicho huku akitoa ahadi ya gari la wagonjwa katika Hospitali ya Murgwanza baada ya kuwasiliana na Waziri wa Afya, Mhe. Jenista Mhagama.

Akizungumzia uchaguzi Mkuu ujao, Askofu Bendankeha amewahimiza wananchi kushiriki kikamilifu na kuwachagua viongozi wao katika uchaguzi Mkuu ujao ili kuchochea maendeleo " Tujiandae kushiriki uchaguzi Mkuu ujao, kura yetu ndiyo nguvu ya mabadiliko." Amesema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mhe. Fatuma Mwassa amelipongeza Kanisa la Anglikana Tanzania kwa huduma mbalimbali za maenseleo zinazotolewa kwa jamii.

# MHANDISI MRAMBA AFUNGUA MAFUNZO YA TEKNOLOJIA YA NISHATI JUA KWA WATAALAM

- Yanahusu usanifu, utengenezaji, ufungaji mifumo ya Nishati Jua na matumizi yake
- Asema mafunzo yanalenga kuendeleza matumizi ya nishati jadidifu kama ilivyoelekezwa katika Dira 2050



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba akifungua mafunzo ya wataalam kutoka taasisi mbalimbali nchini yanayohusu usanifu, utengenezaji na ufungaji wa mifumo ya Nishati ya Jua na matumizi yake.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba amefungua mafunzo ya wataalam kutoka taasisi mbalimbali nchini yanayohusu usanifu, utengenezaji na ufungaji wa mifumo ya Nishati ya Jua na matumizi yake.

Matumizi hayo ni kuchemsha, kupika, kupoza maji pamoja na kukausha mazao kwa kutumia nishati ya Jua.

Akifungua mafunzo hayo jijini Dar es Salaam, Mhandisi Mramba amesema mafunzo kuhusu teknolojia ya nishati ya Jua yanaenda sambamba na vipaumbele vya taifa katika Dira 2050 ambapo Dira hiyo inagusia mikakati ya kuendeleza matumizi ya nishati jadidifu nchini.

"Nishati Jadidifu ikiendelezwa kikamilifu itakuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi, itapunguza utegemezi katika nishati isiyosafi ikiwemo kuni na kuongeza upatikanaji wa huduma za nishati kwa njia ya kisasa zaidi." Amesema Mhandisi Mramba

Mramba amewaasa washiriki wa mafunzo hayo kuwa makini na kuzingatia kile kinachofundishwa ili kiweze kuleta tija nchini.

Vilevile, Mhandisi Mramba ameeleza kuwa Tanzania inajivunia ushirikiano wake na mashirika mbalimbali ya Kimataifa katika kuendeleza Sekta ya Nishati ikiwa ni pamoja na kufanikisha mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo wataalam.

Mafunzo hayo ya Nishati ya Jua yanayojulikana kama SOLTRAIN + yameandaliwa na Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Kituo Mahiri cha Matumizi Bora ya Nishati na Nishati Jadidifu (SACREEE) ambacho kipo chini ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizo Kusini mwa Afrika (SADC).

Jumla ya washiriki 40 kutoka taasisi mbalimbali wanahudhuria mafunzo hayo ya siku mbili wakiongozwa na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga.




Viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati Pamoja na Kituo Mahiri cha Matumizi Bora ya Nishati na Nishati Jadidifu (SACREEE) wakiwa katika picha ya Pamoja.



Jumla ya washiriki 40 katika picha ya Pamoja kutoka taasisi mbalimbali waliohudhuria mafunzo hayo ya Nishati ya Jua (SOLTRAIN) Jijini Dar es salaam

# MWANAMKE NI MSUKUMO WA MAENDELEO KATIKA JAMII - DKT. BITEKO

- Asema Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa wanapata haki na heshima wnayostahili
- Azindua Mpango kazi wa Kitaifa wa Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama
- Unalenga kushirikisha wanawake kikamilifu katika masuala ya Amani na Usalama
- Ataka Wakuu wa Mikoa na Wilaya kutokomeza dalili zinazoweza kuleta uvunjifu wa amani na usalama katika jamii
- Asema kuzinduliwa kwa mpango kazi wa Amani na Usalama kunaonesha jinsi Tanzania inavyoheshimu na kutekeleza makubaliano ya kimataifa



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizindua Mpango kazi wa Kitaifa wa Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema Wanawake ni chanzo cha msukumo wa maendeleo katika Jamii hivyo Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa kila mwanamke nchini awe mama au mtoto wa kike anapata haki na heshima anayostahili.

Wakati Serikali ikiendelea kuhakikisha kuwa Wanawake nchini wanapata haki zao ikiwemo ya usalama na amani, ametoa wito kwao kuendelea kujitambua na kuchangamkia kila aina ya fursa inayojitokeza nchini.

Dkt. Biteko amesema hayo wakati akizindua Mpango kazi wa Kitaifa wa kutekeleza Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama 2025 – 2029 ikiwa ni Azimio namba 1325 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuhusu Wanawake, Amani na Usalama.

Azimio hilo ambalo limeridhiwa na nchi zote Wanachama wa Umoja wa Mataifa ikiwemo Tanzania linasisitiza na kutoa kipaumbele kwenye ushiriki

kamili wa wanawake katika hatua zote za ujenzi wa amani, uzuiaji na utatuzi wa migogoro, mazungumzo ya amani, ulinzi wa amani na ujenzi mpya wa jamii baada ya migogoro.

Dkt. Biteko amesema kuwa kutekelezwa kwa Azimio hilo la Umoja wa Mataifa kunaonesha kuwa Tanzania si nchi inayoridhia tu mipango ya kimataifa inayowekwa bali inaheshimu makubaliano na maazimio ya kimataifa na hii inaifanya Tanzania chini ya uongozi wa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan nikuzidi kuaminika Kimataifa na kuwa mfano wa kuigwa.

Akizungumzia, utekelezaji wa Ajenda hiyo ya Wanawake nchini Tanzania, Dkt. Biteko amesema kuwa "Tanzania tulishapiga hatua kubwa na tunaendelea vizuri katika kutekeleza Ajenda hii ya Wanawake, Amani na Usalama ambapo kwa mujibu wa Gender Inequality Index ya mwaka 2021, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishika nafasi ya 146 kati ya nchi 191 kutokana na maendeleo yaliyopo tangu miaka ya 1990 katika kuhimiza usawa wa kijinsia, uwezeshaji wa wanawake, kubiresha afya ya Mama na Mtoto pamoja na uwepo wa Uwakilishi wa Wanawake Bungeni."

Ameongeza kuwa, mujibu wa Global Peace Index ya mwaka 2021; Tanzania ilishika nafasi ya 58 kati ya nchi 163 zilizo na hali bora ya amani Duniani.

Akieleza kuhusu mafanikio. mengine yaliyofilkiwa katika Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama nchini, Dkt. Biteko amesema Tanzania imeendelea kuwapa Wanawake fursa za juu na za Maamuzi ambapo hadi. kufikia Mei, 2023 Uwakilishi wa Wanawake katika mfumo wa Mahakama umefikia asilimia 46.6.

Ameongeza kuwa asilimia 22 ya Askari Polisi ni Wanawake na asilimia 30 ya Maafisa Uhamiaji ni Wanawake vile vile, Tanzania Bara ina Mawakili wa Serikali 785 ambapo kati yao wanawake ni 410 sawa na asilimia 52.

Ameeleza kuwa kwa upande wa Zanzibar, kuna jumla ya Mawakili wa Serikali 76 ambapo Wanawake ni 34 sawa na asilimia 44 ya Mawakili wote hivyo kwa hatuo hizo zilizopigwa na Tanzania nchi haina budi kujipongeza.

Pamoja na mafanikio hayo, Dkt. Biteko amesema kuwa bado kuna masuala ambayo yanahitaji kupewa msukumo ili kuleta haki na usalama kwa wanawake kwani takwimu zinaonesha kuwa asilimia 48.3 ya wanawake wote Tanzania wamewahi kufanyiwa ukatili wa aina mbalimbali, ambapo mwaka 2015 asilimia 65 ya wanawake waliogombea nafasi mbalimbali za uongozi walikutana na changamoto ikiwemo za matusi huku asilimia 17 ya wanawake hao wakishambuliwa na asilimia 13 wakiombwa rushwa ya ngono.

Amesisitiza kuwa takwimu hizo zinaonesha kuwa bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili kuinua haki ya mwanamke hivyo mpango huo uliozinduliwa unalenga kuhakikisha kuwa matendo yasiyo ya haki kwa wanawake yanatoweka na hadhi ya mwanamke inapanda kuliko sasa.

Aidha, Dkt. Biteko amewataka Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuutekeleza mpango huo wa amani na usalama kwa nguvu kubwa ikiwemo kutoa elimu na kutokomeza dalili zinazoweza kuleta uvunjifu wa amani na usalama ikiwemo mila na desturi zinazoweza kuleta madhara kwenye jamii, wahamiaji haramu, unyanyasaji wa kijinsia na matumizi ya dawa za kulevya.

Kwa upande wake, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dkt. Dorothy Gwajima ametaja baadhi ya vipaumbele vya Mpango wa Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama kuwa ni uzuiaji wa migogoro, ushiriki wa wanawake katika kufanya maamuzi kwenye ngazi zote katika mikataba ya amani na kuwalinda wanawake na wasichana dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia wakati na baada ya migogoro .

Amesema kuwa mpango huo utaleta matokeo chanya kwenye masuala ya amani na usalama kwa wanawake na kuwezesha Serikali kutimiza wajibu wake kitaifa, kikanda na kimataifa katika kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu kwenye masuala hayo ya amani na usalama.

Kwa upande wake, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mhe. Stergomena Tax amesema uzinduzi wa mpango huo ni tukio la historia na lenye uzito si kwa taifa tu bali kimataifa katika kujenga dunia yenye haki usawa na amani.

Ameongeza kuwa, ni kielelezo thabiti cha dhamira ya Serikali katika ushirikishaji wanawake katika masuala ya amani na usalama na uongozi.

Amemshukuru Rais Samia kwa kuwa sauti ya kimataifa katika kuhakikisha kuwa Dunia inakuwa na haki na amani na hii imepelekea Tanzania kutambulika duniani kwa kutoa mchango



Wageni mbalimbali waliohudhuria uzinduzi wa Mpango kazi wa Kitaifa wa kutekeleza Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama 2025 – 2029 ikiwa ni Azimio namba 1325 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuhusu Wanawake, Amani na Usalama.

mkubwa katika misheni za kuleta amani ambapo hadi sasa Tanzania imeshatoa takriban askari 1500 katika misheni za kuleta amani na idadi hiyo ikijumuisha wanawake na wanaume.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Zanzibar, Mhe. Riziki Pembe ameeleza kuwa Mpango wa Ajjenda ya Wanawake, Amani na Usalama uliozinduliwa ni muhimu kwa maendeleo ya wanawake wote na Tanzania kwani maendeleo yanazidi kuchipua pale kunapokuwa na amani na usalama.

Amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatekeleza ajenda hiyo kwa vitendo kwani nafasi za uongozi kwa wananwake zimeongezeka, mfano ukiwa ni uteuzi wa majaji wanawake wasiopungua sita ambapo hapo nyuma idadi ilikuwa chini ya hapo, pia Serikali inazingatia bajeti za masuala ya kijinsia kwa wizara zote.

Naye, Anna Mutavati, Mkurugenzi wa UN- Women katika Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, ameipongeza Tanzania kwa kuzindua ajenda hiyo ya Usalama na Amani kwa wanawake na kueleza kuwa inaendelea kuwa mfano wa kuigwa katika masuala ya amani na usalama ikiongozwa na Amiri Jeshi Mkuu ambaye ni Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

# KASI NDOGO YA UTEKELEZAJI MRADI WA UMEME WA CHALINZE - DODOMA YAMKASIRISHA DKT. BITEKO

- Asikitishwa mradi huo aliouzindua Novemba 2024 kuwa nyuma kwa asilimia Saba
- Asema Rais Samia alitoa agizo mradi usichezewe kutokana na umuhimu wake katika mikoa mbalimbali ikiwemo ya Magharibi
- Asema sababu zilizotolewa na mkandarasi (TBEA) za kusuasua kwa mradi hazikubaliki
- Atoa maagizo kwa Mkandarasi kuwasilisha mpango kazi mpya kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati ili kufidia muda uliopotezwa
- Aagiza TANESCO kutumia mapato ya ndani kulipa fidia wananchi wanaopisha mradi

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amekagua mradi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovolti 400 kutoka Chalinze hadi Zuzu Dodoma na kueleza kutoridhishwa kwake na utekelezaji wa mradi huo ambao ulipaswa kuwa umefikia asilimia 31 lakini kwa sasa umefikia asilimia 24 tangu kuzinduliwa kwake Novemba mwaka 2024.

Hali ya kusuasua kwa mradi imebainika wakati Dkt. Biteko akikagua mradi huo katika Kijiji cha Manchali wilayani Chamwino mkoani Dodoma ambapo Dkt. Biteko amemuagiza mkandarasi kampuni ya TBEA ya China kuhakikisha kuwa anafidia muda wa kazi uliopotezwa wa asilimia Saba ili mradi ukamilike kwa wakati kutokana na umuhimu wake nchini.

Mwezi Novemba, 2024 Serikali ilikubaliana na mkandarasi kuwa mradi huo ufanyike ndani ya miezi 19 tu badala ya miezi 22 kwani wakati mradi unazinduliwa tayari kazi kubwa za awali zilikuwa zimeshafanyika ikiwemo za upembuzi yakinifu na utoaji wa maeneo.



Dkt. Biteko akiwaasa Wananchi kutozuia utekelezaji wa miradi pale inapopita kwenye maeneo yao na Serikali kwa upande wake itahakikisha kuwa wanapata haki wanazostahili .

“ Leo ni miezi saba imepita tangu tuzindue mradi sawa na asilimia 32 ya muda wote tuliokuwa tunahitaji kutekeleza mradi huu, na tulitegemea mradi kwa sasa ufikie asilimia 31 lakini katika hali ya kushangaza mradi umefikia asilimia 24 tu jambo ambalo halikubaliki.” Amesema Dkt. Biteko

Dkt. Biteko ameeleza kuwa, sababu zilizotolewa na Mkandarasi za kuchelewesha mradi ikiwemo ya wananchi kugoma kutoa maeneo kwa madai ya fidia na kukutana na miamba katika mkuza wa mradi hazikubaliki kwani wananchi hao wana haki na lazima walipwe fidia.

Kutokana na hali hiyo, ameagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kutumia mapato yake ya ndani kulipa fidia wananchi waliopisha mradi.

Dkt. Biteko ametanabaisha kuwa mkandarasi alishaagizwa asiutekeleze mradi huo kwa mazoea kutokana na umuhimu wake kwani kwa sasa miundombinu

inayosafirisha umeme kwenda Dodoma kutoka mradi wa Julius Nyerere (JNHPP) kupitia kituo cha Chalinze inabeba umeme kidogo kwa takriban megawati 240 tu ambayo ni sawa na mashine moja tu kati ya mashine 9 za JNHPP hivyo njia hiyo mpya ya umeme ya kV 400 inayojengwa ni muhimu.

Amesisitiza kuwa njia mpya ya umeme ya kV 400 ni muhimu kwani katika Mkoa wa Dodoma mahitaji ya umeme yanaongezka kila siku huku mkoa huo pia ukiwa ni kitovu cha usambazaji umeme katika mikoa yote ya Magharibi ikiwemo Singida, Tabora, Shinyanga Mara na Kigoma ambayo inategemea utulivu wa umeme katika Mkoa wa huo na kwamba Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alishaagiza kuwa mradi huo usichezewe hivyo Mkandarasi ahakikishe kuwa anaupa umakini mkubwa.

Kutokana na mradi huo kuwa nyuma katika utekelezaji, Dkt. Biteko amemuagiza Mkandarasi kuja na mpango mpya wa utekelezaji wa kazi ukiwemo wa kufidia muda uliopotezwa ambapo ametoa siku nne mpango wa fidia ya muda uwasilishwe kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati.

Vilevile, Dkt. Biteko ameagiza mkandarasi kuongeza nguvu kazi ya watu ili minara 917 ya umeme inayopaswa kujengwa kwenye mradi huo ijengwe kwani kwa sasa mkandarasi amechimba takriban mashimo 100 tu kwa ajili ya usimikaji wa minara. Pia amemtaka Mhandisi mshauri wa mradi kuhakikisha anasimamia mradi huo kwa ufanisi na aeleze ukweli pale anapoona kuwa hauendi sawa.

Aidha amemuagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, kutengeneza



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akikaguwa mradi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovolti 400 kutoka Chalinze hadi Zuzu Dodoma na kueleza kutoridhishwa kwake na utekelezaji wa mradi huo ambao ulipaswa kuwa umefikia asilimia 31 lakini kwa sasa umefikia asilimia 24 tangu kuzinduliwa kwake Novemba mwaka 2024.

timu itakayoungana na TANESCO kuusimamia mradi huo na kila wiki taarifa itolewe kuwa umefikia wapi.

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko amewaasa Wananchi kutozuia utekelezaji wa miradi pale inapopita kwenye maeneo yao na Serikali kwa upande wake itahakikisha kuwa wanapata haki wanazostahili kwani Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshaelekeza kuwa hataki wananchi wafanyiwe dhuluma ambapo wasaidizi wake wanahakikisha kuwa agizo hilo linatekelezwa.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule amesema mradi huo wa usafirishaji umeme wa kV 400 kunaenda kuifanya Dodoma kuwa kitovu cha usambazaji umeme nchini.

Aidha, ameahidi kuyasimamia maelekezo yote yaliyotolewa na Dkt. Biteko ya kuhakikisha kuwa mradi huo unakamilika kwa wakati ili kuwezesha umeme huo utakaofikishwa Dodoma, kusambazwa pia kwenye maeneo mengine nchini.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Lazaro Twange amesema Mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma unakusudia kusafirisha umeme wote unaozalishwa kutoka katika Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (Megawati 2,115) na kuingiza kwenye gridi ya Taifa kisha kuufikisha kwenye maeneo yote yenye mahitaji ya umeme.

Amesema mkataba na mkandarasi kampuni ya TBEA ulisainiwa mwaka 2024 na mradi kuanza kutekelezwa mwezi Novemba 2024 ambapo mkandarasi ameshalipwa awamu ya kwanza ya malipo ambayo ni shilingi za kitanzania bilioni 107 na mhandisi mshauri ameshalipwa asilimia 15 ya malipo yake.

Ameeleza kuwa maagizo yote yaliyotolewa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati yatafanyiwa kazi ikiwemo ya kuhakikisha kuwa mradi unakamilika mwezi Juni au kabla ya Juni 2026 kwa mujibu wa mkataba.

Aidha, Ameishukuru Serikali chini ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa shilingi bilioni 513 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ambao utakuwa na urefu wa kilometa 345 na kuhusisha minara ya umeme ipatayo 917 kutoka Chalinze mkoani Pwani hadi Zuzu mkoani Dodoma.

# WATUMISHI WAHIMIZWA KUJENGA MAKAZI KABLA YA KUSTAAFU

- Wasisitizwa kuzingatia Maadili ya Utumishi wa umma
- Mramba apongezwa kwa kutatua Changamoto za Watumishi



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, akiwahimiza watumishi wa umma kutumia fursa zilizopo katika taasisi za kifedha kwa ajili ya kujiimarisha kiuchumi, ikiwemo kujenga makazi yao binafsi kabla ya kustaafu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, amewahimiza watumishi wa umma kutumia fursa zilizopo katika taasisi za kifedha kwa ajili ya kujiimarisha kiuchumi, ikiwemo kujenga makazi yao binafsi kabla ya kustaafu.

Ushauri huo umetolewa wakati Katibu Mkuu huyo alipokutana na wafanyakazi wa wizara hiyo katika kikao cha ndani kilichofanyika jijini Dodoma.

“Tumieni fursa ya mikopo



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Peter Mataragio akizungumza na watumishi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati.



Picha ya Pamoja watumishi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati waliohudhuria katika kikao hicho.

inayotolewa na taasisi za kifedha nchini ili mjenge maisha yenu mapema. Msisubiri hadi mstaafu ndipo muanze kufikiria kujenga nyumba ya kuishi," alisisitiza Mhandisi Mramba.

Aidha, alikumbusha watumishi kuendelea kuzingatia maadili ya utumishi wa umma kwa kuwa na nidhamu, weledi, na kuepuka vitendo vya rushwa, sambamba na kutunza mali za serikali kama kompyuta na vifaa vingine vya ofisi.

"Serikali inatumia gharama kubwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kazi kwa ajili ya kuwahudumia wananchi. Ni wajibu wetu kuvithamini na kuvitumia kwa tija," aliongeza.

Katika kikao hicho, watumishi walimpongeza Katibu Mkuu kwa utaratibu wake wa kuwa karibu nao kwa kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili, hatua waliyoieleza kuwa imeongeza hamasa na uwajibikaji kazini.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Peter Mataragio, Wakuu wa Idara na Vitengo kutoka wizara hiyo pamoja na watendaji kutoka taasisi mbalimbali za serikali.

# SHIMIWI NI MAHALA PA KAZI – Bi ZIANA MLAWA

- Asema Wizara ya Nishati ipambane irudi na ushindi
- Asema Wizara ya Nishati iwe mfano kwa Wizara zingine



Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Nishati, Bi. Ziana Mlawa akizungumza na watumishi ambao ni washiriki wa michezo mbalimbali alipokuwa akiwaaga wakielekea kushiriki michezo ya SHIMIWI itakayofanyika jijini Mwanza.

Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Nishati, Bi. Ziana Mlawa amesema kushiriki michezo mbali mbali inasaidia katika kujenga afya ya mwili na akili hivyo mtumishi anapopata nafasi ya kushiriki michezo yeyote aitumie ipasavyo pia husaidia hali itakayowajengea uwezo kujiamini zaidi ikiwemo katika maeneo ya kazi.

Bi. Mlawa ameyasema hayo alipokuwa akiwaaga watumishi wa Wizara ya Nishati watakao shiriki michezo ya SHIMIWI itakayofanyika jijini Mwanza kwanzia tarehe 1 Septemba, 2025.

" Pamoja na kushiriki michezo ambapo ni mbali na eneo la kazi mkumbuke mkiwa huko ni eneo la kazi nidhamu na uadilifu uwe kipau mbele mdaa wote muwapo kwenye michezo hiyo." Amesisitiza Bi. Mlawa

Ameongeza kuwa watumishi hao wajitahidi wapate ushindi ambapo kwa ushindi huo Wizara itapata heshima njee na ndani ya Wizara.



Picha ya Pamoja ya washiriki wa michezo ya SHIMIWI wakiagana na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Nishati, Bi. Ziana Mlawa.

# WIZARA YA NISHATI NA TAASISI ZAKE ZASHIRIKI MAONESHO YA KIMATAIFA YA KILIMO DODOMA

Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini yake zinashiriki Katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo maarufu kama ''nane nane'' ambayo yamefanyika Katika Viwanja Nzuguni Jijini Dodoma. Maonesho hayo yalibebwa na kaulimbiu ya " Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo,Mifugo na Uvuvi 2025",

Katika maonesho hayo ambayo yalifunguliwa na Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isdor Mpango,

Watalaam wa Wizara pamoja na kueleza mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Nishati ikiwemo ukamilishaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere na Usambazaji wa Umeme Vijijini, wanatoa elimu kuhusu Nishati Safi ya Kupikia

Aidha wananchi wanafahamishwa kuhusu mipango mbalimbali ambayo Wizara imepanga kutekeleza katika mwaka wa fedha 2025/2026 ikiwemo kuendelea kusambaza umeme vitongojini na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia.

Taasisi za Wizara ya Nishati zinazoshiriki maonesho hayo ni Shirika la Umeme Tanzania ( TANESCO), Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli ( PURA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania ( TPDC), Wakala wa Nishati Vijijini ( REA) Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) na Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania ( TGDC).

Bi. Mlawa ameyasema hayo alipokuwa akiwaaga watumishi wa Wizara ya Nishati watakao shiriki michezo ya SHIMIWI itakayofanyika jijini Mwanza kwanzia tarehe 1 Septemba 2025.

“ Pamoja na kushiriki michezo ambapo ni mbali na eneo la kazi mkumbuke mkiwa huko ni eneo la kazi nidhamu na uadilifu uwe kipau mbele mdaa wote muwapo kwenye michezo hiyo.” Amesisitiza Bi. Mlawa

Ameongeza kuwa watumishi hao wajitahidi wapate ushindi ambapo kwa ushindi huo Wizara itapata heshima njee na ndani ya Wizara.













Wizara ya Nishati Pamoja na Tasisi zake kwenye maonesho ya nane nane katika picha za matukio mbalimbali

# SERIKALI YAIMARISHA MIUNDOMBINU YA CNG KATIKA HARAKATI ZA KULETA MAPINDUZI YA NISHATI

- Vibali vya ujenzi wa vituo vya CNG kutolewa haraka ili kuvutia wawekezaji
- Taasisi za kifedha zashauriwa kutoa mikopo kwa wawekezaji kwenye sekta ya gesi
- Kituo cha Puma Tegeta kuwa kituo kikubwa zaidi cha CNG Jijini Dar es Salaam na Afrika
- Serikali kuanza kutumia magari yanayotumia gesi ya CNG badala ya dizeli na petroli



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati anayeshughulikia Mafuta na Gesi, Dkt. James Mataragio, akieleza hayo wakati wa ziara ya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa vituo vya CNG Jijini Dar es Salaam.

Katika juhudi za kuiwezesha Tanzania kupiga hatua katika matumizi ya gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG) kwa ajili ya magari, Serikali kupitia Wizara ya Nishati inaendelea kuimarisha upatikanaji wa miundombinu muhimu, ikiwemo ujenzi wa vituo vipya vya kujaza gesi kwenye magari katika maeneo mbalimbali.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati anayeshughulikia Mafuta na Gesi, Dkt. James Mataragio, ameeleza hayo wakati wa ziara ya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa vituo vya CNG Jijini Dar es Salaam.

"Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na taasisi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na maji safi (EWURA) na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) imeweka mikakati madhubuti kuhakikisha usambazaji wa gesi ya CNG unafanyika kwa kasi, ikiwemo kuboresha mfumo wa utoaji wa vibali vipya vya ujenzi wa vituo ili vipatikane haraka," alisema Dkt. Mataragio.

Alisisitiza kuwa hatua hiyo inalenga kuwavutia wawekezaji wengi zaidi na kuharakisha upatikanaji wa huduma hiyo katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, alibainisha kuwa dhana iliyokuwepo awali miongoni mwa baadhi ya wawekezaji kuwa uwekezaji kwenye sekta ya nishati ni wa gharama kubwa na wenye hatari imeanza kubadilika, kufuatia juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje.

Vilevile, alizihimiza taasisi za kifedha, hususan benki, kuendelea kutoa mikopo kwa wawekezaji waliopo katika sekta ya gesi, akisisitiza kuwa soko lina mahitaji makubwa na urejeshaji wa mikopo

hiyo utakuwa rahisi kutokana na faida inayopatikana katika biashara hiyo.

Katika ziara hiyo, Dkt. Mataragio alikagua maendeleo ya ujenzi wa vituo vya CNG vilivyopo maeneo ya Tegeta (Puma), Goba (BQ) na Tanzania State Natural Gas), Mwenge (Enego Energies), Tan Health (Africana) na kituo cha TPDC kilichopo Hospitali ya Taifa Muhimbili ambacho ujenzi wake umekamilika, pia amesema kuwa vituo hivyo vinajengwa na wakandarasi Wazawa

Alieleza kuwa ujenzi wa vituo hivyo uko katika hatua za mwisho, na vinatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu. Kati ya vituo hivyo, kituo cha Tegeta kinachosimamiwa na Kampuni ya Puma kimetajwa kuwa kitakuwa kituo kikubwa zaidi Jijini Dar es Salaam na Afrika, chenye uwezo wa kuzalisha futi za ujazo milioni 6.7 za gesi ya CNG kwa siku.

Pamoja na hayo, Dkt. Mataragio alisisitiza dhamira ya Serikali kuhamasisha wananchi kuachana na magari yanayotumia dizeli na petroli, na badala yake kuanza kuagiza magari yanayotumia gesi asilia.

"Tunaamini matumizi ya gesi ni ya gharama nafuu na salama kwa mazingira, na yanaleta tija kwenye taifa. Wizara ya Nishati itakuwa mfano kwa taasisi nyingine za serikali kwa kutumia magari yanayoendeshwa kwa gesi ya CNG," aliongeza.

Aidha Dkt. Mataragio amesema wizara ya itaandaa warsha ya kuwakutanisha wadau wote wanaohusika katika Biashara ya CNG ikiwemo taasisi za kifedha, Wawekezaji ( Sekta binafsi) na taasisi za umma ili kuwajengea uweelewa kuhusu Biashara ya CNG na Min LNG.

Ziara hiyo ilihudhuriwa pia na wataalamu kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

# ELIMU YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA YAWAFIKIA WANAWAKE MKOANI MBEYA

- Ni kupitia Kongamano la Wanawake na Fursa za Kiuchumi
- Wizara ya Nishati yasisitiza matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ili kulinda afya na mazingira

Serikali kupitia Wizara ya Nishati imetoa wito kwa wananchi kuachana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia na kutumia nishati safi ya kupikia kama vile umeme na gesi ikiwa ni njia pia ya kulinda afya, mazingira na kuimarisha uchumi wa kaya.

Wito huo umetolewa leo na Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia kutoka Wizara ya Nishati, Ndg. Deo Alex katika Kongamano la Wanawake na Wajasiriamali kuhusu fursa za kiuchumi lililofanyika mkoani Mbeya.

Ndg. Deo Alex amesema kuwa mwaka 2022 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alitoa maelekezo ya kuandaliwa kwa



Ndg. Deo Alex akimwakilisha Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia kutoka Wizara ya Nishati katika Kongamano la Wanawake na Wajasiriamali lililohusu fursa za kiuchumi lililofanyika mkoani Mbeya.

Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ikiwa ni mwanzo wa safari ya kuelekea katika matumizi ya nishati iliyosafi ya kupikia.

Ameeleza kuwa kufuatia agizo hilo, Wizara ya Nishati iliandaa mkakati huo na kuuzindua rasmi mwaka 2024 ambapo utekelezaji wake umeanza rasmi.

Ameeleza kuwa, kwa mujibu wa mkakati huo, matumizi ya nishati isiyo safi yameonekana kuwa chanzo kikuu cha athari mbalimbali, ikiwemo uharibifu wa mazingira na matatizo ya kiafya kwa watumiaji, miongoni mwa athari za kiafya zilizobainishwa ni pamoja na saratani, homa za mapafu, ujauzito kuharibika na kujifungua watoto kabla ya muda.

Ameeleza kuwa gharama za kumtibu mtu mwenye saratani ni kubwa ukilinganisha na gharama ya ununuzi wa nishati safi ya kupikia kama vile mtungi wa gesi, hivyo wananchi wanahimizwa kuwekeza katika matumizi ya nishati salama kwa ajili ya afya zao na mazingira,

Ndg. Alex amebainisha kuwa mkakati huo umefungua fursa mbalimbali kwa wajasiriamali, ikiwa ni pamoja na kuwa mawakala wa gesi na nishati nyingine mbadala.

Amezitaja aina za nishati safi zinazopendekezwa kuwa ni pamoja na umeme, gesi na mkaa mbadala.

Wanawake mbalimbali waliohudhuria Kongamano hilo kwa nyakati tofauti wameishukuru Wizara ya Nishati kwa kuwapa elimu hiyo ya Nishati Safi ya Kupikia na kutoa wito kuwa iendelee hadi ngazi ya vijiji.

Kongamano hilo limeandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, likiwa na kauli mbiu isemayo "Changamkia Fursa, Jenga Leo na Kesho Yako."



Picha ya Pamoja washiliki mbalimbali katika kongamano la wanawake na wajasiriamali mkoani Mbeya.

# TUKITUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA TUTAOKOA HEKTA 400,000 ZA MISITU ZINAZOTEKETEA KWA MWAKA-MJIOLOJIA NSAJIGWA

- Awanoa Wanawawake na Wajasiriamali Songwe kuhusu Nishati Safi ya Kupikia
- Atoa wito kwa Wadau kushirikiana na Wizara ya Nishati kutoa elimu ya Nishati Safi ya Kupikia

Imeelezwa kuwa matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia si tu yanahatarisha afya bali pia yanachochea uharibifu wa mazingira ambapo takribani hekta 400,000 za misitu hupotea kila mwaka nchini kutokana na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa, jambo linalochangia kuongezeka kwa ukame na mabadiliko ya tabianchi.

Hivyo, Watanzania wameaswa



Mjiolojia Nsajigwa akiwanoa Wanawawake na Wajasiriamali Songwe kuhusu Nishati Safi ya Kupikia.

kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia na kuachana na matumizi ya nishati isiyo safi kama kuni na mkaa kutokana na athari zake kwa binadamu na mazingira.

Wito huo umetolewa na Mjiolojia kutoka Wizara ya Nishati, Nsajigwa Maclean, wakati akitoa elimu ya Nishati Safi ya Kupikia kwa Wajasiriamali mkoani Songwe.

Amesema kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, ni asilimia 16 tu ya Watanzania ndio wanaotumia nishati safi ya kupikia, hivyo bado kuna magonjwa yanayotokana na moshi wa kuni na mkaa, ambayo yanasababisha vifo vya zaidi ya watu 33,000 kwa mwaka nchini.

Katika ngazi ya kimataifa, amesema watu bilioni 2.1 hawana upatikanaji wa nishati safi ya kupikia, huku zaidi ya watu milioni 3 wakifariki dunia kila mwaka kutokana na madhara ya kiafya yanayotokana na nishati isiyo safi ya kupikia ambapo Kusini mwa Jangwa la Sahara zaidi ya watu milioni 960 hawana nishati hiyo.

Aidha amebainisha kuwa kuna dhana potofu miongoni mwa jamii kuwa chakula kinachopikwa kwa kutumia gesi au umeme hakiwi na ladha nzuri, jambo ambalo amesema halina msingi wa kisayansi na linaendelea kuwazuia wananchi wengi kufanya mabadiliko kuelekea matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Ameeleza kuwa Wizara ya Nishati imeweka mkakati wa kitaifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ili kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2034 asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia, huku mkakati huo ukiangazia mafanikio kutoka nchi nyingine kama India na Ghana, ambazo zimepiga hatua katika kuhimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Imeelezwa pia kuwa changamoto kubwa kwa wananchi si kutotaka kutumia nishati safi ya kupikia bali wanahitaji elimu pia kuhusu matumizi ya nishati hiyo hivyo ametoa wito kwa Wadau kushirikiana na Serikali katika kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa Nishati Safi ya Kupikia.

Katika semina hiyo wanawake na wajasiriamali walihimizwa kuwa mabalozi wa mabadiliko kwa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia si kwa ajili ya afya pekee, bali pia kwa ajili ya kulinda mazingira na kizazi kijacho.

# REA YAZIDI KUHAMASISHA NISHATI SAFI, YATOA BILIONI 4.37 KWA JESHI LA KUJENGA TAIFA

- JKT yaipongeza REA utekelezaji wa miradi ya nishati safi
- REA yaiwezesha JKT asilimia 76 ya miradi ya nishati safi
- Watumishi 7,000 wa JKT kupatiwa Mtungi wa kilo 15 wa LPG pamoja na Jiko lake la sahani mbili kila mmoja
- Anglikana Waishukuru Serikali, washirika wa maendeleo

Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imeendelea kuwezesha, kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa watumishi na askari wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili kufikia malengo yaliyoainishwa kwenye mkakati wa kitaifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia (2024 – 2034).

Hayo yamebainishwa na Kaimu Mkuu wa Tawi la Utawala wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa niaba ya Mkuu wa JKT, Kanali Juma Mrai wakati akifungua mafunzo kwa washiriki toka vikosi 22 vinavyonufaika na mpango wa nishati safi JKT katika bwalo la vijana 834KJ (Makutupora) jijini Dodoma

"Hii yote ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jumhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhusu taasisi zote zinazohudumia watu zaidi ya 100 zihame kutoka katika matumizi ya nishati chafu na kuhamia katika nishati safi ya kupikia, " Ameongeza Kanali Mrai.

Aidha, ameipongeza REA kwa kuhamasisha na kuwezesha matumizi ya nishati safi ili kutunza mazingira na kuepuka



Zoezi la upikaji chakula kwa kutumia Nishati safi likiendelea kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ili kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa watumishi na askari wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili kufikia malengo yaliyoainishwa kwenye mkakati wa kitaifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia (2024 – 2034).

athari za kiafya zinazohusiana na utegemezi mkubwa wa nishati isiyo kuwa safi

"REA imeiwezesha JKT kwa asilimia 76 Sawa na Shilingi Bilioni 4.37 ya utekelezaji wa nishati safi katika kambi 22 za JKT kwa kuzipatia mashine za kutengeneza mkaa Mbadala 60, majiko banifu 291, mifumo ya gesi ya LPG 180 na masufuria yake, Mkaa Mbadala tani 220, mafunzo kwa vijana 50,000 pamoja na mifumo ya Gesi Vunde 9 " Amesisitiza Kanali Mrai.

Aidha, ameipongeza REA kwa kuhamasisha na kuwezesha matumizi ya nishati safi ili kutunza mazingira na kuepuka athari za kiafya zinazohusiana na utegemezi mkubwa wa nishati isiyo kuwa safi

"REA imeiwezesha JKT kwa asilimia 76 Sawa na Shilingi Bilioni 4.37 ya utekelezaji wa nishati safi katika kambi 22 za JKT kwa kuzipatia mashine za kutengeneza mkaa Mbadala 60, majiko banifu 291, mifumo ya gesi ya LPG 180 na masufuria yake, Mkaa Mbadala tani 220, mafunzo kwa vijana 50,000 pamoja na mifumo ya Gesi Vunde 9 " Amesisitiza Kanali Mrai.

Katika hatua nyingine, amewataka watendaji waliolengwa kutumia mashine za kutengeneza mkaa mbadala, majiko banifu na majiko ya gesi pamoja na mkaa rafiki wa mazingira unaotokana na mabaki ya mazao ya shambani kupatiwa elimu ili kuwa na uwezo wa kubaini na kutatua changamoto za nishati hiyo na hatimaye bidhaa hizo kuleta tija kwa taifa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Teknolojia za Nishati Jadidifu na Mbadala kutoka REA, Mha. Advera Mwijage amesema mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo maafisa na askari wa vikosi vilivyopo katika mpango wa REA ili waweze kuwa mabalozi wazuri wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwenye maeneo yao ya kazi.

Ameongeza kuwa mafunzo hayo yatachangia katika mlolongo mzima wa kuwa na matumizi endelevu ya Nishati Safi ya Kupikia kwa sababu mafunzo haya yanatoa fursa ya kupata ujuzi utaowawezesha Kusimamia mifumo ya Nishati safi vizuri.

Aidha Amelipongeza Jeshi la Kujenga Taifa kwa utekelezaji mzuri wa mradi na kuahidi ushirikiano katika kuhakikisha tunakamilisha mradi huu kwa wakati.

Katika hatua nyingine, Mha. Mwijage amebainisha kuwa, tayari REA imeidhinisha zaidi ya milioni 800 kwa ajili ya watumishi 7,000 wa JKT kupatiwa Mtungi wa kilo 15 wa LPG pamoja na Jiko lake la sahani mbili kila mmoja ikiwa ni sehemu wa kuhamasisha matumizi ya Nishati safi ya Kupikia kwa mtu mmoja mmoja.


For more info
www.nishati.go.tz
The United Republic of Tanzania
Ministry of Energy
ANNOUNCEMENTS
EVENTS